KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA

# Sera ya KKKT ya Mawasilano

## UTANGULIZI

**TASWIRA**

Ushirika wa watu wenye upendo, amani na furaha waliobarikiwa kiroho na kimwili, wenye matumaini ya kuurithi uzima wa milele kwa njia ya Yesu Kristo.

**DHAMIRA**

Kuwafanya watu wote wamjue Yesu Kristo ili wawe na uzima tele, kwa kuwahubiria Habari Njema kwa maneno na matendo, kwa kuzingatia Neno la Mungu kama ilivyo katika Biblia na msingi wa Mafundisho ya Kilutheri kwa kuongowa na Katiba ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

**TAFSIRI**

Sera ya mawasiliano ni mkusanyiko wa kanuni na viwango vilivyowekwa kuongoza mwenendo na jinsi vyombo vya mawasiliano vitakavyofanya kazi. Sera inafafanua malengo, shabaha na wajibu wa vyombo vya mawasiliano vya Kanisa. Mawasiliano katika Kanisa na kati yake na wengine duniani yanatakiwa kuimarishwa ili kutimiza wajibu na misioni ya Kanisa vizuri.

Ni muhimu katika kipindi cha kuendea Karne mpya kuhakikisha kuwa viongozi wa Kanisa na washarika kwa ujumla wamejiandaa kutumia ipasavyo vyombo na teknologia mpya ya habari na mawasiliano ili kuboresha huduma mbalimbali za Kanisa.

Sera ya Mawasiliano itasaidia Kanisa linalokuwa haraka kama KKKT kuwa na mipango mizuri na kuongeza ufanisi wa miradi ya mawasiliano.

## SABABU ZA KIBIBLIA

Vigezo muhimu vya mawasiliano ya Kikristo:

**a) Ni Kitu Ambacho Kipo Tangu Awali**

Ili tujenge mahusiano tunawasiliana na Mungu wetu pia, (Walawi 19:18). Tunapowasiliana ndipo tunaitika wito wetu na kwamba sote tu waangavu na dhaifu kwa kuwa maisha yetu yana mwisho.

**b) Ni Utume au Unabii**

Kwa kuwasiliana kwa mbinu na njia mbalimbali, Kanisa lisikilize sauti za wanyonge wanaoonewa, lijihusishe na yanayotendeka katika jamii na kusaidia ‘sauti za wasio na sauti’ zisikike na mara zote litoe changamoto katika kutekeleza wajibu wake wa utume na unabii, (Warumi 12:2).

**c) Ni Lazima Yalete Ukombozi au Mabadiliko**

Bwana Yesu ambaye ni asili ya mawasiliano kati ya mwanadamu na Mungu alisema: “Nanyi mkikaa katika Neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kwelikweli, tena mtaifahamu, nayo hiyo kweli itawaweka huru,’’ Yohana 8:31-32.

**d) Liingize Mafunzo ya Demokrasia**

Kristo alipowasiliana na wengine hakutoa mahubiri peke yake bali aliruhusu mazungumzo kwa njia ya kuuliza maswali na kutaka watu wamuulize maswali, (Luka 10:29).

**e) Yatetee Maendeleo ya Kijamii**

Mawasiliano yasiwe ni sauti isiyo na lengo maalum, nia iwe ni kujenga mahusiano na wengine. Chombo cha Kanisa cha mawasiliano kiwe ni kichocheo cha maendeleo sio tu kwa lengo la kusaidia kuondoa umaskini bali hata kukomboa watu kiakili, kimwili na kiroho. Matumizi ya neno “Yetu” katika Sala ya Bwana ni kielelezo kuwa maisha katika jamii yatakamilika endapo kuna mawasiliano, (Mathayo 6:6-13; Luka 11:2-4).

## UENDESHAJI WA VYOMBO VYA HABARI

Vyombo vya habari huendeshwa kwa kamati ya uhariri /au ya utangazaji.

**KAMATI ZA UHARIRI/ UTANGAZAJI**

Kiongozi wa Kituo/ Mhariri anakuwa kiongozi wa kamati ya uendeshaji.
Wakuu wa vitengo/ idara katika chombo cha habari kinacho husika wanakuwa wanakamati.

**KAZI ZAKE**

- Kazi ya kwanza ya kamati ni kuandaa mipango kwa ajili ya vipindi vya redio /TV au kuandaa misuada ya maandiko husika.
- Kufuatilia utekelezaji wa kazi zilizopangwa.
- Kamati inawajibu wa kusimamia sera ya utangazaji au maandiko, kutoa miongozo ya utendaji kazi na inapobidi wanakamati wanatakiwa wafunike kisichotakiwa kusambazwa (censorship).
- Kamati pamoja na kufanya vikao na kuongoza pia inafanya kazi za uhariri.

- Kamati inawajibu kuhakiki vipindi vya redio au TV, muziki, maneno ya muziki, taarifa za habari na matangazo yote. Na kwa upande wa maandiko katika majarida, nk., kamati inapaswa kuhakiki taarifa na misuada kabla ya kuitangaza au kuichapisha.

## NAFASI MUHIMU KWA MUUNDO WA VYOMBO VYA HABARI

- Mhariri/ Mkurugenzi wa Kituo cha Redio au TV
- Mkuu wa Mafundi kwa redio na TV
- Mhariri Msanifu/ Msimamizi wa Vipindi
- Mkuu wa Masoko/ Mauzo au Matangazo ya Biashara.

## SERA NDOGO YA UHARIRI NA UTANGAZAJI (EDITORIAL / BROADCASTING POLICY)

Sera ya Uhariri na Utangazaji ni kitu kinachopaswa kuwa katika maandishi na kijulikane kwa kila utumishi wa vyombo vya habari. Kwa kawaida huwa na vipengele vifuatavyo:

**Tamko la Misioni ya KKKT**

- Sera ya Ndogo ya Uhariri na Utangazaji (Broadcasting and Editorial Policy) ni kitu muhimu kwa mujibu wa Sheria za nchi.
- Tamko la misioni la KKKT linaelezwa namana litakavyo tekelezwa na kituo au gazeti husika.
- Tamko linaelezea maudhui, madhumuni, malengo, taswira au maono na misioni ya Kanisa kwa ujumla lakini kituo/ gazeti linatoa tafakari ya kiutendaji.

**Maelezo Muhimu ya Utambulisho**

- Ni muhimu maelezo mafupi kuhusu mambo muhimu ya utambulisho wa gazeti au kituo cha utangazaji yawepo katika sera hiyo ndogo. Kwa mfano:
- Gazeti litatolewa mara ngapi au muda wa kurusha matangazo ya redio/ au TV ni upi?
- Gazeti litakuwa na safu gani au vipindi na saa zipi stesheni ya redio/ TV itakuwa wazi?
- Gazeti linafika maeneo gani au redio/ TV inatangaza katika masafa na mita bendi gani?

**Wajibu wa Viongozi Wakuu Unawekwa Bayana**

Kugawana majukumu kwa njia ambayo yupo anaye wajibika kuhakiki na kuchuja (censorship) taarifa kwa mujibu wa sheria za nchi, kanuni zinazoongoza taasisi husika na kufafanua wajibu wa utii kwa watumishi wa Kanisa na kujenga mahusiano.

**Ufafanuzi wa Maana na Dhana Mbalimbali**

- Ni muhimu kutoa ufafanuzi wa dhana muhimu kwa usahihi (accuracy);
- kutopendelea (objective) na
- kutoa nafasi sawa ya kujieleza (balance).

**Hiki ni Chombo cha Mahusiano**

- Hutumika kujenga mahusiano kwa hiyo mtazamo/ msimamo kwa mujibu wa misioni na sera za Kanisa utawekewa mkazo.
- Upendeleo, propaganda, fafanuzi na tafakari yenye lengo la kujenga imani kwa mujibu wa mafundisho ya Kilutheri utatamkwa wazi wazi.
- Tunajaribu kuinua mafundisho gani? Kwa nini kisitumiwe kujenga madhehebu tofauti na letu? nk.
- Mawasiliano ni kuuza: Je, tunauwafikishia ujumbe gani watu wengine?
- Chombo hiki ni kwa ajili ya kulea jamii kimwili, kiroho na kiakili
- Chombo hiki kisitumike na yeyote kupotosha njia.

## MUONGOZO WA UTENDAJI (STYLE-BOOK)

Huu ni mwongozo muhimu kwa ajili ya watumishi wote wa vyombo vya habari. Style-book ni kama ‘Biblia’ ya taasisi au chombo cha habari. Lakini baadhi ya mambo katika huo mwongozo yananaweza kurekebishwa inapoonekana haja ya kufanya hivyo. Mwongozo huo una mambo makuu yafuatayo:

- Unaeleza namna ya kutenda kazi za kila siku katika chombo cha habari husika, k.m. kuandaa vipindi, nk.
- Unafafanua jinsi ya kukusanya taarifa, nani wa kushirikiana naye, nk.
- Unagusia wajibu kwa Kanisa (loyalty /allegiance) na kuwajibika kwa taifa (responsible coverage).
- Unaeleza wazi wazi mambo ya kufanya, kwa mfano: Lengo la chombo hicho cha Kanisa ni kueneza Injili na kuinua mafundisho ya Kiluteri.
- Unaagiza kuhusu vyeo (titles) na ufupisho (abbreviations) utakavyo paswa kutumika hewani ama katika maandiko husika.
- Mwongozo huo unaeleza kwa kifupi miiko ya watumishi wa vyombo vya habari kwa mujibu wa Sheria za nchi, taratibu za Kanisa na maadili ya taaluma yenyewe.

## MAWASILIANO YALIYOPO

**Mawasiliano Katika Dayosisi**

Mawasiliano kati ya dayosisi moja ya KKKT na nyingine hufanywa kwa *barua za posta, simu za kiganjani na za mezani, telefax, barua pepe, sms, WhatsApp, mikutano, warsha, mafunzo, taarifa kwa njia ya vyombo kama redio, tovuti, majarida nk.* Viongozi wa Kanisa liweka utaratibu wa mtandao wake wa mawasiliano ya mara kwa mara ya kuunganisha Kanisa zima kwa njia ya

barua zinazotumwa kama barua pepe. Kwa kuwa Kanisa lina miradi kama: nishati jadidifu; tiba mtandao (tele-medicine); *barua pepe, simu za kiganjani, tovuti na* njia za miradi mbalimbali pamoja na ile ya kijamii kama mkongo wa mawasiliano wa kitaifa; vyote hivi vitumike kwa ukamilifu zaidi ili kuimarisha mawasiliano katika Kanisa. Kwa kufanya hivyo tutatekeleza lengo la kuimarisha umoja wa Kanisa pia.

**Majarida Katika Kanda**

Kanisa lina gazeti la Uhuru na Amani katika ngazi ya Kanisa. Dayosisi zifuatazo zina magazeti/majarida mbalimbali kama vile:

a) Dayosisi ya Kaskazini Magharibi - Ija Webonere
b) Dayosisi ya Kaskazini Mashariki - Njia
c) Dayosisi ya Kaskazini - Umoja
d) Dayosisi ya Mashariki na Pwani - Upendo
e) Dayosisi ya Kusini - Njoo Uone
f) Dayosisi ya Iringa - Dira

Kutokana na uwezo mdogo wa raslimali katika Idara za Mawasiliano za Dayosisi ingefaa Dayosisi ziwe na magazeti ya kanda ambayo yatasambazwa katika dayosisi nyingine pia.

**Radio Sauti ya Injili**

Makanisa dada na washirika mbalimbali ikiwa ni pamoja na Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), yanasaidia kuanzisha Kituo cha kurekodi matangazo ya Radio Sauiti ya Injili (SYI) kwa masafa mafupi (SW) na baadaye kituo kilianza matangazo ya masafa mafupi (FM) tangu 1994. Dayosisi ya Iringa ina Kituo cha Redio kiitwacho Radio Furaha, Dayosisi Mashariki na Pwani ina Kituo cha Redio na Gazeti lenye jina Upendo na Dayosisi ya Kaskazini Mashariki ina kituo cha Redio Utume.

Vipindi vya SW vya SYI vilikuwa vikirushwa hewani kupitia mitambo ya TransWorld Radio toka Manzini, Swaziland. Vipindi vya FM vinapata misaada toka wadau mbalimbali likiwemo Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Bavaria, Ujerumani. Ni kwa kuona hatari ya kuendelea kutegemea ufadhili mkubwa toka nje ndio sababu iko haja ya kuanzisha miradi ya pamoja ya mawasiliano kwa kubuni na kufikiri zaidi kuhusu fursa zilizopo ili kuondokana na mtindo wa kila idara/ vituo au dayosisi kutoa huduma zinazofanana kwa walengwa wale wale badala ya kushirikiana.

Sera hii pia inalenga kuhamasisha washarika kufahamu umuhimu wa mawasiliano kama nyenzo au raslimali muhimu inayopaswa kufanyiwa maandalizi vizuri kabla ya kutolewa, kudhibitiwa, kusimamiwa na kutawanywa kwa manufaa ya Kanisa zima. Kila msharika anawajibika kutoa/ kupokea habari kwa usahihi na kusahihisha taarifa yo yote ambayo inapotosha ukweli.

## WAJIBU WA VYOMBO VYA HABARI VYA KANISA

Wajibu wa vyombo vya habari na ofisi za uhusiano za KKKT ni:

- Kutangaza Injili kwa mapana yake kwa mujibu wa misioni ya Kanisa.
- Kuunga mkono na kutangaza maadili, taswira, misioni, sera na malengo ya Kanisa.
- Kusaidia kurahisisha utoaji maamuzi kwa mambo yanayohusu Kanisa.
- Kusaidia kurahisisha upatikanaji habari za shughuli za Kanisa.
- Kutekeleza jukumu la haki ya kupashana habari zinazohusu mambo yatakayo athiri maisha ya watu katika jamii.
- Kutoa fursa ya mchango wa mawazo ya wengine kuhusu masuala ya Kanisa.
- Kuimarisha umoja na kusaidia washarika watambue umuhimu wa kuwa na mshikamano katika Kanisa.
- Kuwa mawakili wa amani, umoja wa kitaifa, uzalendo na kutambua mamlaka za kitaifa.

Wajibu huu wenye vipengele nane uwekwe pamoja kama mwongozo wa kuendesha kila chombo cha mawasiliano cha Kanisa yaani magazeti au majarida, vitabu, maandiko mbalimbali na vituo vya utangazaji kama Radio na Televisheni.

## MAWASILIANO KATIKA KARNE MPYA

KKKT inathamini na kutambua baraka inayotokana na hatua kubwa ya maendeleo iliyopigwa katika mawasiliano kimataifa. Tupo katika enzi za kuwasiliana kwa kutumia *satellite* inayounganisha mtandao wa kompyuta duniani (Internet). Viongozi wa Kanisa watahakikisha hawakwepi teknologia hiyo bali wananunua vifaa kama kompyuta na kuzitumia kikamilifu ili kuwaletea mabadiliko washarika kwa kuhakikisha malengo ya Kanisa yanafikiwa kwa ufanisi zaidi. Maendeleo katika mawasiliano ni zawadi toka kwa Mungu, kwa hiyo, sote tuhakikishe tunaitumia vizuri zawadi hiyo kwa utukufu wake.

Kwa kuwa huwezi kuwa na Kanisa imara na endelevu bila vyombo na ofisi imara za mawasiliano, hivyo kila Dayosisi, taasisi, na ofisi za Kanisa ziwe na vitengo vya habari /mawasiliano /uhusiano vilivyo na raslimali za kuviwezesha kufanyakazi zake vizuri kuepuka migongano na jamii au watumishi wake.

Kwa kuwa Mkuu wa KKKT ndiye msemaji wa Kanisa Dayosisi, taasisi za Kanisa nazo zinahimizwa kupashana taarifa za kimaendeleo kutoka maeneo yao ili kutangaza mchango wa kanisa katika jamii na kujenga umoja wa Kanisa.

## MAFUNZO YA MAWASILIANO

Mafunzo ya mawasiliano yawekwe kwenye mipango yote ya mafunzo katika Kanisa. Ni muhimu yaingizwe katika mitaala ya masomo katika Vyuo vikuu, vyuo vya Biblia, Seminari (Lutheran Junior Seminary), madarasa ya Elimu ya Kikristo, Shule za Msingi na hata Sekondari, kwa ujumla. Sharika zitumike kama vituo vya huduma za komputa kwa vijana na watumishi wa kanisa.

Mawasiliano liwe ni somo la lazima katika mafunzo ya elimu ya theologia ili Wachungaji wapewe stadi za kutumia vyombo vya mawasiliano ili kutimiza wajibu wao kwa ufanisi zaidi. Masomo hayo yatasaidia wajiandae vema zaidi kutoa mahubiri yanayojibu masuala yanayohusu jamii wanayoihudumia.

Maelezo na miongozo itolewe kwa makundi mbalimbali kama ya vijana na wanawake kuanzia Dayosisi hadi sharikani kwa nia ya kujenga mahusiano mazuri katika makundi hayo yawasiliane mara kwa mara, nk. Tangu sharikani hadi dayosisi vitumike

vyombo vya kuwasiliana kulingana na mazingira na raslimali kutegemea uwezo. Mawasiliano huweka huru, kwa hiyo mawasiliano yasaidie kutambua na kuwaweka huru wanaoteseka katika jamii.

Maoni au marejesho yanayoonyesha malalamiko yanaweza kuashiria mgogoro utakaojitokeza karibuni. Mgogoro unapotokea ama washarika wengi wanapoacha kuwa washiriki, kwa mfano, Kanisa/ Dayosisi/ Sharika inabidi kuchukua hatua ili kujua kama upo ufa kati ya uongozi na wale wanaoongozwa. Ubunifu uwepo katika matumizi ya vyombo muafaka vya kuwasiliana, mfano vipeperushi kila mwezi badala ya kuwa na matangazo marefu katika Ibada zetu. Pia kanisa ngazi zote litumie barua pepe, sms, au vyombo vya habari inapofaa ili kukuza umoja amani na maelewano katika jamii.

Madhumuni ya semina/kozi za mawasiliano kwa vikundi mbalimbali kama wanawake na vijana yawe ni kwa ajili ya kuwahamasisha watumie vyombo vya mawasiliano kubadilishana mawazo, uzoefu au kuhimiza mambo ya kujengana katika nyanja za kiroho, kiakili na namna ya kujikomboa toka umaskini.

Viongozi na watumishi ngazi zote kuanzia Sharika, Majimbo, Dayosisi, vituo vya na ofisi za kanisa wapitie mafunzo ili wawe mstari wa mbele kuwaandaa wakristo kutambua hazina iliyopo katika kupata stadi za kutumia mbinu za mawasiliano ikiwa ni pamoja na ujuzi wa kutumia kwa ufanisi vyombo vya kisasa vya habari na mawasiliano.

Vijana waandaliwe kutoa huduma katika fani ya mawasiliano katika Kanisa kwa kutiwa moyo kujiunga na masomo ya mawasiliano hadi Chuo Kikuu. Ni ukweli usiopingika kuwa, watu waliolelewa na kupewa mafunzo na Kanisa wanatii wanakapoitwa kulitumikia Kanisa.

Kwa kuwa Kanisa lina Chuo Kikuu cha Tumaini, Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa na Chuo Kikuu cha Iringa, vyuo hivi na matawi yake vinapewa changamoto ya kuwa Mafunzo ya Mawasiliano kwa viwango cha shahada, pia mafunzo maalumu (tailor-made courses)ya muda mfupi kwa makundi mbalimbali kutokana na mahitaji.

## KITENGO CHA NYARAKA
## (Documentation Clearing House)

Kanisa liwe na kitengo kidogo chenye ufanisi kitakachokusanya, kuandaa na kutoa nyaraka, taarifa rasmi, taarifa zilizofanyiwa upembuzi yakinifu na ripoti za utafiti kuhusu shughuli za Kanisa na jamii kwa ujumla. Pia kijihusishe na kuandaa taarifa zinazotakiwa katika ndani au nje ya kanisa na ndani au nje ya nchi.